



MAJI TANZANIA

1 - 5 - 7 - 5 Tupo Site Kikazi Zaidi



Toleo 033

Julai - Septemba 2026

Haliuzwi

Serikali imejipanga na kujidhatiti kuhakikisha miundombinu ya Majisafi na Majitaka nchini inaendelea kutoa huduma kwa ufanisi kuelekea msimu wa Mvua zilizotabiriwa za El-nino kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA).

Uk. 03



Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba ametaka miradi yote ya maji inayojengwa nchini izingatie shughuli za kilimo kwa ajili ya umwagiliaji na kuhakikisha kunakuwa na mabwawa kwa ajili ya kunyweshea Mifugo.

Uk. 02



MIRADI YA MAJI IZINGATIE KAZI ZA KILIMO NA UFUGAJI

Nanenane , Dodoma

Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba ametaka miradi yote ya maji inayojengwa nchini izingatie shughuli za kilimo kwa ajili ya umwagiliaji na kuhakikisha kunakuwa na mabwawa kwa ajili ya kunyweshea Mifugo.

Amesema hayo Mkoani Dodoma akifungua maonesho ya kimataifa ya Kilimo ya Nane Nane yenye kauli mbiu "Tambua soko ongeza tija kutekeleza Dira 2050".

" Nadhani tulimsikia Waziri wa Maji Mh. Jumaa Aweso (Mb) akisema miradi yote inayoendelea nchini, ikiwemo na Mradi mkubwa wa Gridi ya maji ya Taifa inazingatia pia shughuli za Kilimo na ufugaji, na mimi nasisitiza kama kuna eneo kuna mitambo ya kuchimbia mabwawa basi pia itumike kuchimbia mabwawa kwa ajili ya kunyweshea Mifugo" Mhe. Dkt. Nchemba amesema.

Maonesho ya Kilimo ya Nane nane yamefunguliwa katika viwanja vya Dkt John Malecela vilivyopo Nzuguni Jijini Dodoma ambapo Wizara ya Maji imeshiriki sambamba na Taasisi zilizo chini yake ikiwemo DUWASA, RUWASA, Mfuko wa Taifa wa Maji na Bodi ya maji ya bonde la Wami-Ruvu.





MAJI TUMEJIWEKA TAYARI NA MVUA ZA EL- NINO

- AWESO

Dar es Salaam, **Tanzania**

Serikali imejipanga na kujidhatiti kuhakikisha miundombinu ya majisafi na majitaka nchini inaendelea kutoa huduma kwa ufanisi kuelekea msimu wa Mvua zilizotabiriwa za El-nino kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA).

Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) amesema hayo wakati akikagua miundombinu ya majisafi na majitaka ya Jiji la Dar es salaam ikiwa ni lengo la kuhakikisha serikali ina utayari na tahadhari za mvua za El-nino zinazotarajiwa hivi karibuni.

Waziri Aweso ametembelea Mto Mpiji uliopo Mabwepande eneo linapopita mabomba makubwa ya maji ya inchi 72" na 54" yanayohudumia asilimia hamsini ya wakazi wa mkoa wa Dar es salaam na mkoa wa Pwani, pia amekagua bohari ya vifaa ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) kuona utayari na changamoto zozote zitakazojizokeza wakati wa mvua hizo ili wananchi wa Dar es salaam na Pwani waendeleo kupata huduma ya maji pamoja na mvua hizo kubwa.

Amekagua miundombinu ya majitaka katika eneo la Mwenge na daraja la Salenda ambapo ameziagiza mamlaka za maji nchini kujidhatiti katika utoaji wa huduma ya maji hasa kuhakikisha madawa ya kutosha ya kutibu maji yapo kuelekea kwenye msimu wa Mvua za El-nino na kuhakikisha miundombinu ya majitaka katika maeneo yao inakua katika hali nzuri ili mvua zisisababishe kuzagaa kwa majitaka mtaani.

Ameridhishwa na maandalizi yanayofanywa na DAWASA kama tahadhari kuelekea kwa msimu wa Mvua za El-nino.





SERIKALI KUIMARISHA UBORA WA MAZINGIRA KWA MRADI WA MBEZI BEACH

Mbezi, Dar es Salaam

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kimeridhishwa na ujenzi wa Mtambo wa Kisasa wa Kuchakata Majitaka unaojengwa na Serikali kupitia Mradi wa Usafi wa Mazingira Mbezi Beach jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Jackson Kiswaga (Mb), amesema ni mtambo mkubwa na wa kisasa wa kuchakata majitaka ukanda wa Afrika Mashariki, akisisitiza ni matokeo ya uwekezaji mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha usalama wa mazingira na afya za wananchi.

"Kamati itaishauri Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kupata maeneo mengine ya kujenga mitambo kama hii, kutokana na ongezeko la watu na ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam, niwasihi wananchi wanaonufaika na mradi huu kujitokeza kuunganishwa na mfumo wa majitaka na kuacha utiririshaji holela majitaka kuchafua mazingira na kuhatarisha afya za wakazi" Mhe. Kiswaga amesema.





Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amesema mradi huo wa kimkakati umetumia teknolojia ya kisasa itakayoweza uchakataji wa majitaka na uzalishaji wa bidhaa muhimu ikiwemo mbolea na gesi. Amesema teknolojia hiyo pia imezingatia mazingira ya wananchi wanaoishi jirani na mtambo, hivyo hawataathiriwa na hali ya hewa mbaya.



"Serikali inaendelea na miradi mingine ya kimkakati ya uchakataji wa majitaka, ikiwemo Mradi wa Buguruni, utakaonufaisha zaidi ya wakazi 100,000 katika kata 12 za Kinondoni na Ilala lengo ni kuhakikisha asilimia 80 ya majisafi yanayogeuka kuwa majitaka yanapata sehemu ya kuhifadhiwa na kuchakatwa vyema bila kuathiri Mazingira" Mhe. Aweso amesema.

Mbunge wa Jimbo la Kawe Mhe. Geoffrey Timothy (Mb) ameshukuru Serikali kwa utekelezaji wa mradi huo, na kusema changamoto ya kina cha maji chini ya ardhi kuwa juu katika eneo la Mbezi Beach imekuwa ikisababisha mashimo ya majitaka kujaa mara kwa mara na baadhi ya wananchi kuyatiririsha uchafu mitaani.

"Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuondoa changamoto hiyo na kuimarisha afya na usafi wa mazingira kwa wananchi lakini pia kutapunguza gharama za maisha kwa wakazi wengi, mradi utakapokamilika mwananchi hatakuwa tena na sababu ya uchafuzi wa Mazingira" Mhe. Geoffrey amesema.

Mradi wa Usafi wa Mazingira Mbezi beach unatekelezwa na Wizara ya Maji kupitia DAWASA unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2026 utanufaisha kaya zaidi ya 11,000 katika kata nne za Wilaya ya Kinondoni ambazo ni Kawe, Kunduchi, Mbezi Juu na Wazo.



WATENDAJI SEKTA YA MAJI WATAAKIWA KUACHA ALAMA

Dodoma, Tanzania

Watendaji wa Sekta ya Maji wametakiwa kuacha alama katika utendaji wao kwa kuzingatia matokeo, uwajibikaji na ubora wa huduma za maji kwa kila mwananchi.

Wito huo umetolewa wakati Serikali ikiimarisha utaratibu wa uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora unaolenga maslahi ya wananchi.

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb.), ametoa wito huo katika hafla ya utiaji saina wa mikataba ya utendaji kati ya Wizara ya Maji, Bodi za Maji za Mabonde na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini iliyofanyika jijini Dodoma..

Waziri Aweso amesema mikataba iliyotiwa saina ni ahadi ya uwajibikaji na ufanisi kwa watendaji katika kutekeleza majukumu yao ili kufanikisha malengo na vipaumbele vya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Amewataka watendaji wa taasisi zote za Sekta ya Maji kutimiza malengo waliyojiwekea kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma.

Amebainisha kuwa rasilimali za maji ni suala la usalama wa taifa, na kuitaka Bodi ya Taifa ya Maji pamoja na Bodi za Maji za Mabonde kusimamia, kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya sasa na ya baadaye.

“Bodi za Maji za Mabonde zinatakiwa kuwa na mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa takwimu sahihi za rasilimali za maji, kwani ndiyo msingi wa kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya sekta na taifa kwa ujumla,” amesema Waziri Aweso.

Aidha, amezitaka Mamlaka za Maji kuboresha huduma zake.

Amesisitiza kuwa mwaka wa fedha 2026/27 ni mwaka wa kuongeza kasi kiutendaji kupitia uboreshaji wa mifumo ya utawala bora, upunguzaji wa malalamiko ya wateja, uongezaji wa uzalishaji wa maji, udhibiti wa upotevu wa maji na uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi.



Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amesema Sekta ya Maji inagusa moja kwa moja maisha ya wananchi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Ameongeza kuwa vipimo vya utendaji kazi vitatumika kama kigezo cha kupima uwezo na ufanisi wa watendaji kuendelea kubaki katika nafasi zao.



Zanzibar, Tanzania

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mhe. Dkt.Hussein Ali Mwinyi** akiwa Ikulu ya Zanzibar, alipokutana na Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Zanzibar, **Mhe. Nadir Abdullatif**, pamoja na ujumbe wa Waziri wa Maji wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Jumaa Aweso (Mb)**.



SERIKALI YASISITIZA USHIRIKIANO NA SEKTA BINAFSI (PPP)

Bungeni, Dodoma

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amesisitiza umuhimu wa kuimarisha Ushirikiano kati Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) katika kuongeza uwekezaji na kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maji nchini.



Ameyasema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya Wizara ya Maji katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kipindi cha miaka mitatu, kuanzia mwaka 2024 hadi 2025.

Waziri Aweso amesema Serikali inaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha rasilimali zinatumiwa kwa ufanisi, sambamba na kushirikisha sekta binafsi na

wadau mbalimbali katika kuongeza uwekezaji na kuboresha huduma za maji nchini.

Amesisitiza umuhimu wa kukamilisha miradi ya maji vijijini, kwasababu Serikali inalenga kumaliza uhaba wa maji katika vijiji 1,575 ambavyo bado havijafikiwa na miundombinu ya huduma ya maji.

Waziri Aweso amesisitiza matumizi bora ya fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kuzielekeza katika maeneo yenye mahitaji makubwa, na kutaka utekelezaji wa miradi uzingatie thamani ya fedha kwa kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa manufaa ya wananchi.





WIZARA YA MAJI YAWASILISHA MPANGO WA GRIDI YA TAIFA YA MAJI KWA KAMATI YA BUNGE

Bungeni, Dodoma

Wizara ya Maji imewasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) akiwasilisha taarifa hiyo kwa niaba ya Waziri wa Maji amesema utekelezaji huo ulishaanza kwa kutekeleza miradi mikubwa ya maji ambayo inatumia vyanzo vya uhakika vya Maji ikiwemo mradi wa maji ya ziwa Victoria ambayo yamefika Shinyanga hadi wilaya za mkoa wa Tabora na kazi ikiendelea kufikisha maji Dodoma.

Amesema Gridi ya Taifa ya Maji ambayo ni kichocheo kikubwa cha kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2050 unatarajiwa kuwa na mtandao wenye urefu wa zaidi ya Km 6200 ambao utahusisha mitaro ya wazi zaidi ya Km 1200 na mabomba zaidi ya Km 5000.

Mradi huo utatekelezwa kwa awamu tatu hadi kukamilika kwake mwaka 2050.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Jackson Kiswaga (Mb) amepongeza na kutaka uzingatiaji wa mahitaji yote ya maji kwa matumizi ya nyumbani, mifugo na mimea.





MFUKO WA TAIFA WA MAJI WATAKIWA

KUTAFUTA VYANZO MBADALA VYA FEDHA

Koloni, Dodoma

Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) umetakiwa kutumia ubunifu kupata vyanzo mbadala vya fedha kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika kikao kazi na watumishi wa NWF jijini Dodoma leo Septemba 4, 2026 amewataka kuwa wabunifu kutafuta vyanzo mbadala vya fedha ili kufanikisha miradi ya maji ya kimkakati ambayo itakuwa kielelezo katikwa kuchochea maendeleo

“Tumefanya vizuri kupitia hati Fungani ya Kijani ya Tanga UWASA sasa ni muda wa kuwa na Hati Fungani ya kifedha inayotolewa kwa ajili ya kugharamamia miradi ya maji” (Water Infrastructure Bond), Waziri Aweso amesema..

Ameitaka Menejimenti ya NWF na watumishi wa taasisi hiyo kutekeleza maelekezo hayo kwa vitendo, ubunifu na uwajibikaji ili kuongeza mchango katika kufanikisha nia ya serikali ya kutoa huduma ya maji iliyo bora, salama, toshelevu na endelevu.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri katika kikao hicho amesema ili kuchochea mabadiliko watumishi wa taasisi hiyo wanatakiwa kufanya kazi kwa umoja na ushirikiano kwa kuzingatia

Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma ikiwamo utunzaji wa siri na nyaraka mbalimbali za serikali.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Maji, Wakili Haji Nandule amesema maelekezo yaliyotolewa katika kikao atahakikisha yanafanywa kazi kwa wakati na kusimamia utekelezaji wake.

Mfuko wa Taifa wa Maji ni taasisi ya Serikali iliyopo chini ya Wizara ya Maji inayotekeleza Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya 2019, ikikusanya na kusimamia fedha za miradi ya maji, uhifadhi wa vyanzo vya maji na uboreshaji wa huduma ya maji katika jamii nchini Tanzania,





RUWASA WAKABIDHIWA CHETI CHA ITHIBATI ISO 9001:2015

Dodoma, Tanzania

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limekabidhi cheti cha ubora wa huduma kwa Wakala ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ikiwa ni ishara ya utoaji huduma bora ya maji nchini.

Hafla hiyo imefanyika jijini Dodoma Septemba 2026 ambapo Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS Mhandisi Abadallha Killeo amesema kuwa utoaji wa cheti cha ubora ni hatua kwani cheti hicho kinatolewa baada ya ukaguzi, upimaji pamoja na kuhakikisha vigezo vya ubora vinafikiwa.

Cheti hicho cha Ubora kimekabidhiwa na kushuhudiwa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika siku ya ufungaji wa Kikao kazi cha siku tatu kwa watendaji na Menejimenti ya RUWASA jijini Dodoma.

Waziri wa Maji Mhe. Aweso alitumia nafasi hiyo kuwapongeza RUWASA kwa kufanikiwa kupata cheti cha ithibati namba ISO 9001:2015. “Kupata cheti ni jambo moja, uwajibikaji ni suala la Pili, naomba mhakikishe mnaendelea kusimamia ubora wa huduma kwa wananchi” Mhe. Aweso amesema.

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Walter Kirita alimhakikishia Mhe. Waziri Aweso na viongozi wengine taasisi hiyo itaendelea kusimamia utoaji huduma bora

kwa wananchi ambao ndio walengwa katika utendaji wa kila siku.

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini RUWASA inahudumia Mikoa 25 nchini katika Wilaya 128 ambapo mpaka Desemba 2025 huduma ya upatikanaji wa maji Vijijini ilifika asilimia 85.2 kutoka asilimia 64 iliyokuwepo wakati RUWASA inaanzishwa mwaka 2019. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 RUWASA imepanga kutumia shilingi Bilioni 188 ambapo kiasi cha shilingi Bilioni 41 imepangwa kuanzisha miradi mipya katika vijiji 400 nchini.

Kikao hicho cha siku tatu kiliongozwa na kauli mbiu inayosema “kutoka ujenzi wa Miradi hadi Utoaji Huduma ya Maji ya Uhakika kwa wananchi Vijijini”





MKANDARASI BWAWA LA KIDUNDA ATAHADHIRISHWA KUJIANDAA NA MVUA ZA EL NINO

Kidunda, Morogoro

Mkandarasi anayetekeleza ujenzi wa bwawa la Kidunda ametahadharishwa na uwezekano wa uwepo wa mvua za El Nino mwishoni mwa mwaka 2026.

Mwenyekiti Bodi ya Maji ya Taifa, Bwn. Suffian Ally ametoa tahadhari hiyo kwa mkandarasi kampuni ya Sino Hydro Corporation, kwa kuzingatia kwa karibu utabiri wa hali ya hewa katika utekelezaji wa mradi



Amesema utabiri umeonesha uwezekano wa mvua za El nino kunyesha mwishoni mwa mwaka

2026 hivyo aweke mpango kazi ambao hautaathiriwa na hali hiyo.

Bw. Ally ameongoza wajumbe wa Bodi hiyo kutembelea mradi wa Kidunda unaolenga kupambana na upungufu wa huduma ya maji



Ameongeza maendeleo ya mradi huo yanaridhisha lakini ujenzi haupaswi kusimama kwa kisingizio cha mvua bali kufanya maandalizi mapema ili kukabiliana na hali hiyo.

Naye Katibu wa Bodi hiyo ambaye pia ni Mkurugenzi Rasilimali za Maji Wizara ya Maji, Bw. Robert Sunday amempongeza Rais wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia vizuri mapato ya ndani ambayo yamewezesha kutekelezwa kwa mradi huo. Amesema wazo la ujenzi wa mradi huo lilianza zaidi ya mika 50 iliyopita hadi Rais Dkt. Samia alipoamua kulitekeleza kwa kutumia fedha za ndani.





Amesema ni uthubutu ambao unapaswa kupongezwa na kila Mtanzania na kuwahakikishia Watanzania kuwa mradi huo utakamilika na kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo jirani.

Kwa upande wake Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu Nickson Lutenda amesema vyanzo vyote vya maji vinavyotiririsha maji katika bwawa hilo vitaendelea kulindwa ili kuwezesha uendelevu wa bwawa nakusisitiza wananchi wajiandae kuchangamkia fursa

zinazotokana na bwawa hilo ikiwemo kilimo na ufugaji.

Bwawa la Kidunda linatekelezwa kwa fedha za ndani zaidi ya shilingi bilioni 300. Ujenzi wake umefika asilimia 52.4



SEKTA YA MAJI KATIKA UBORA, TANGA UWASA

YANYAKUA TUZO C-CEOs FORUM 2026

Arusha, Tanzania

Sekta ya Maji imechomoza kwa taasisi zake tatu kuibuka kwa kufanya vizuri ambapo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) imeibuka mshindi wa kwanza na kutunukiwa Tuzo katika kipengele cha Shirika la Umma la Kibiashara lililofanya vizuri zaidi katika Menejimenti ya

Rasilimali-Fedha, kupunguza matumizi na kuongeza ufanisi katika urejeshaji wa mtaji. Taasisi nyingine ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) ambazo zipo katika orodha ya taasisi zilizofanya vizuri.

Tuzo hiyo imetolewa wakati wa Kikao Kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma (C-CEOs Forum 2026), kilichofanyika katika Ukumbi wa Arusha International Conference Centre (AICC), Arusha.





Makamu wa Rais, Mhe. Deo Ndejembu, ametoa pongezi kwa Tanga UWASA kwa kutambuliwa kwa utendaji wake, akisisitiza umuhimu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kuendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali, kuongeza ufanisi na kuhakikisha yanatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa.



Mafanikio hayo yanaendelea kuonesha umuhimu wa usimamizi bora wa rasilimali katika Taasisi na Mashirika ya Umma, hususan katika kuimarisha ufanisi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.



DODOMA YAPATA MRADI WA KUTHIBITI UPOTEVU WA MAJI

Bahi, Dodoma

Mradi wa majaribio wa mfumo wa uwiano wa maji (water balance) umezinduliwa wilaya ya Bahi, Dodoma, ukiwa na thamani ya shilingi bilioni tisa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amezindua mradi huo kwa niaba ya Waziri wa Maji.

Amesema teknolojia ya kupima kiasi cha maji yanayotumika katika eneo (DMAs – District Metered Devices/Areas) itatumika kubaini uzalishaji na matumizi ya maji.

Ameeleza kuwa mradi huo utakuwa mfano kwa nchi nzima katika utoaji wa huduma na kudhibiti maji yanayopotea (Non-Revenue Water – NRW).

Mhandisi Mwajuma amesisitiza kuwa kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha huduma ya maji ya uhakika na endelevu inawafikia wananchi.





Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania, Mhe. Ahn Eun Ju, amesema nchi yake inasimama na Tanzania katika kufanya kazi pamoja ili jamii inufaike, ikiwemo kupata huduma ya maji ya uhakika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, amefafanua kuwa wakazi 437,200 wa Bahi na Dodoma mjini watanufaika na huduma hiyo.

Mradi huo unafanikishwa na Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na Serikali ya Korea Kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA) na unahusisha ufundi, ujenzi na kujenga uwezo kwa wataalamu wazawa, na unatekelezwa katika eneo la huduma la DUWASA.

**SERIKALI IMEFANIKISHA
KAZI YA KUCHIMBA
VISIMA 10 MKOANI
SINGIDA KWA KUTUMIA
WATAALAM WAZAWA
NA MITAMBO YA
SERIKALI**



Singida, Tanzania

Serikali imefanikisha kazi ya kuchimba visima 10 mkoani Singida kwa kutumia wataalam wazawa na mitambo ya Serikali.

Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) kufuatia kazi hiyo amemkabidhi mkandarasi kampuni ya Megha Engineering and Infrastructure, visima hivyo kukamilisha utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28.

Singida ni moja ya miji mitatu katika mkoa wa Singida inayonufaika na mradi wa maji wa miji 28.

Waziri Aweso ametoa siku 15 kwa mkandarasi huyo kukamilisha kazi ya usanifu wa mradi na utekelezaji kuanza mwezi Oktoba 2026.





TANZANIA YAZINDUA JUKWAA LA NANE LA

WADAU WA MAENDELEO YA BONDE LA MTO NILE

Dodoma, Tanzania

Jukwaa la Nane la Wadau wa Maendeleo ya Bonde ya Mto Nile (NBDF8) limezinduliwa rasmi nchini Tanzania.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amefanya uzinduzi huo jijini Dodoma kwa niaba ya Waziri wa Maji.

Lengo la jukwaa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano wa nchi washirika wa Bonde la Mto Nile katika kutafuta suluhisho bunifu za kugharamia miundombinu ya maji na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhandisi Mwajuma amesema Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa jukwaa akisisitiza kuwa Tanzania ni mshirika muhimu katika bonde hilo hasa kutokana na ukweli kuwa Mto Nile chanzo chake kikubwa ni ziwa Victoria ambalo sehemu yake ipo Tanzania

Ameeleza kuwa Bonde la Mto Nile linakabiliwa na changamoto zinazoongezeka kwasababu ya mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la idadi ya watu na matumizi, ukuaji wa uchumi pamoja na mahitaji makubwa ya maji, chakula na nishati.

Ukuaji huo unasukuma umuhimu wa nchi wanachama kushirikiana katika kulinda, kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji zinazoshirikishwa.

Ametaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na ushiriki wa Tanzania katika Bonde hilo kuwa ni pamoja na kuboreshwa kwa vituo vinane vya kitaifa vya ufuatiliaji wa taarifa za maji katika Bonde la Ziwa Victoria, matumizi ya teknolojia za kisasa za mawasiliano katika ukusanyaji wa taarifa za maji pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kufuatilia ubora wa maji, na maji chini ya ardhi, pamoja na nishati ya umeme.





Jukwaa hilo litatekelezwa kupitia shughuli mbalimbali zitakazojumuisha uwasilishaji wa tafiti, semina za mtandaoni, kampeni za uhamasishaji wa umma na mkutano wa mkuu utakaofanyika Dar es Salaam, ambapo itafanyika mijadala ya kitaalamu, majadiliano ya viongozi mbalimbali. Aidha amewaalika wataalamau wa maandiko na waandishi wa habari kushiriki kwa kuwasilisha habari na maandiko ambayo yatashindanishwa na kupata tuzo.

Mtendaji Mkuu wa Jukwaa la Bonde la Nile Mhandisi Nestor Niyonzima ametoa wito kwa wadau mbalimbali kushiriki katika kuwasilisha maandiko na habari mbalimbali ambazo zinazohusu Bonde la Mto Nile kwa lugha mbalimbali, ikiwamo Kiswahili.

USALAMA WA MAJI WAJADILIWA KISEKTA

Bungeni, Dodoma



Dodoma, Tanzania

Wizara Ya Maji imefanya majadiliano na Benki ya Dunia kuhusu program ya usalama wa maji nchini.

Majadiliano yamefanyika katika mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma na kuongozwa na Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Wizara ya Maji Bw. Robert Sunday.

Mazungumzo yamefanyika mahsusi kuongeza ushirikiano na serikali ili kubaini vipaumbele vya

uwekezaji na kuimarisha ushirikiano wa baadae katika eneo la kuimarisha usalama wa maji nchini.

Majadiliano yatasaidia kuweka Sekta ya Maji kama kichocheo cha uchumi mpana badala ya kuwa sekta ya huduma katika jamii pekee kwa kuunganisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na mahitaji ya maji safi, uzalishaji wa chakula, nishati, maliasili, miundombinu na uhifadhi wa mazingira.





"SERIKALI INAWAJALI WATUMISHI SANA" - AWESO

Dodoma, Tanzania

Serikali inaendelea kuhakikisha maeneo ya kazi kwa watumishi wa umma ni salama ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya kiwango.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika kikao na watumishi wa Wizara ya Maji Sepetmba 2026 katika ukumbi wa Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma amesema Serikali itasimamia maslahi bora kwa watumishi na sio maneno.



"Tufanye kazi vizuri na kwa ubora, mimi nitawapigania katika kazi ili Sekta ya Maji itimize lengo la Serikali" Waziri Aweso amesema na kusesitiza ni vizuri kila mtumishi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo mbalimbali ya serikali.

Waziri Aweso amesema na kuwataka watumishi kujivunia kazi kubwa wanayofanya na wawe walimu popote watakapokuwa kuhusu utekelezaji wa kazi na kufikisha huduma ya maji katika jamii.

Amesisitiza watumishi kukumbuka familia pamoja na majukumu wanayotekeleza kwa kusesitiza ***"Mwenda kwao haogopi giza"*** kwa sababu kuijali familia ni baraka ya Mwenyezi Mungu ambayo ataweka wepesi katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

Waziri Aweso amewakumbusha watumishi wote kuishirikisha jamii katika kazi ili kuwa na uelewa wa pamoja na manufaa ya kazi kujulikana mapema katika jamii.

Mhe. Aweso amesainisha vipaumbele nane kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kuwa ni pamoja na kukamilisha uandaaji wa Mpango mkuu wa rasilimali za maji nchini, ukamilishaji wa mchakato wa matumizi ya Dira janja, utafutaji wa vyanzo mbadala vya Fedha, utekelezaji wa Gridi ya Taifa ya Maji, uanzishwaji wa makavazi ya wizara, mpango wa kufikisha maji ya ziwa Victoria Dodoma na kuwa na Ramani mahsusi ya mtandao wa mfumo wa maji kwa Sekta ya Maji nchi nzima.

"Ili kutimiza malengo haya lazima tuhakikishe sisi kama viongozi tunawatengenezea watumishi wetu mazingira mazuri ya kazi na ile dhamira ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani inatimia" Aweso amesema.

Pamoja na hayo amewataka wataalamu kuhakikisha mifumo yote ya Taasisi za wizara inasomana na wizara ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi.





Dodoma, Tanzania

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Bi. Rose Ambrose leo Septemba 29, 2026 amefanya ziara ya kutembelea na kushuhudia zoezi la matengenezo ya visima vilivyopata changamoto katika chanzo kikuu cha Maji Mzakwe eneo la Mamba jijini Dodoma.

Bi. Rose ametoa maagizo ya kuhakikisha visima vyote vyenye changamoto vinakamilika kwa wakati na haraka ili wananchi waweze kupata maji ya uhakika.

Pia Bi Rose ameitaka DUWASA kuhakikisha wanakuwa na pampu na mota za ziada ili kuweza kusaidia kipindi visima vinapopata changamoto yeyote hasa katika kipindi hiki cha mategemeo ya mvua kubwa za El Nino.



Kwa upande wa Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira DUWASA, Mhandisi Bernard Rugayi amesema kuwa watahakikisha kazi zote zinakamilika kwa wakati ili huduma iweze kuimarika kwa wananchi.

Naibu Katibu Mkuu ametembelea kisima namba C3 ambacho ameshuhudia matengezo yake kukamilika na

kisima kuanza kufanya kazi. Pia ametembelea visima namba 147 na C6 ambavyo matengenezo yake yanaendelea. Visima vyote hivyo viko Mzakwe eneo la Mamba.





SERIKALI YASISITIZA USIMAMIZI IMARA WA MAJI CHINI YA ARDHI

Dodoma, Tanzania

Serikali imezitaka kampuni na wadau wote wanaojihusha na utafiti na uchimbaji wa maji chini ya ardhi kuzingatia utaratibu wa kuwa na nyaraka halali za sheria, leseni na kukidhi viwango vya kitaalamu ili kulinda rasilimali hiyo muhimu kwa maendeleo na usalama wa taifa.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akifungua Warsha ya Wadau wa Maji Chini ya Ardhi ya mwaka 2026 jijini Dodoma, amesema maji chini ya ardhi ni akiba ya kimkakati inayosaidia kuhakikisha upatikanaji wa maji safi, hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Amesema uchimbaji holela wa visima unahatarisha ubora na uendelevu wa rasilimali hiyo, hivyo Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi, utoaji wa leseni na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika usimamizi wa sekta.

Amewataka wadau kushiriki kikamilifu katika kampeni ya **“1575 Tupo Site Kikazi Zaidi”**, inayolenga

kuhakikisha vijiji vilivyosalia vinapata huduma ya uhakika ya maji kwa ushirikishwaji wa sekta binafsi.

Ameelekeza Wizara ya Maji kuboresha kanzidata ya visima, kuanzisha mfumo wa kidigitali wa utoaji wa leseni na vibali, kuimarisha mafunzo ya wataalamu pamoja na kuanzisha Umoja wa Wadau wa Maji Chini ya Ardhi ili kuimarisha weledi, uwajibikaji na ushindani wa kiwango.





CHAMWINO WALIPWA FIDIA BILIONI 4.9

KUPISHA CHANZO CHA MAJI

Chamwino, Dodoma

Serika imelipa fidia kiasi cha Shilingi bilioni 4.9 kwa wananchi wilayani Chamwino waliopisha eneo la hifadhi ya maji Chamwino.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) akikabidhi mfano wa hundi kwa wawakilishi wa wananchi hao amesema maji ni kichocheo cha maendeleo na kusesitiza, chanzo cha Chamwino ni muhimu kwa Jiji la Dodoma na maeneo jirani.

Amesema fidia hiyo inalipwa kwa wananchi 880 ili kuhakikisha chanzo hicho kinalindwa kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Amesema bila kulinda vyanzo vya maji, upatikanaji wa maji wa uhakika hauwezi kufikiwa kwasababu mamlaka za maji zitakuwa na miundombinu isiyokuwa na faida kwa jamii.

Ameainisha kuwa Serikali imelipa wananchi jumla ya Shilingi bilioni 36.756 iliwa ni fidia katika maeneo mbalimbali ya hifadhi ya maji nchini.

Amezielekeza Bodi za Maji za Mabonde kuhakikisha vyanzo vya maji vinasimamiwa, vinawekewa mipaka na kutangazwa rasmi, na kuzitaka mamlaka za maji kushirikiana na mabonde kuhakikisha maeneo hayo yanapatiwa hati miliki na kuwekewa mikakati ya kudhibiti uvamizi na ushirikishwaji wa wananchi katika ulinzi wa miundombinu.

Amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, itaendelea kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amesema historia ya eneo hilo ni kuwa lilitangazwa kuwa eneo la hifadhi mwaka 1973, likiwa na ukubwa wa ekari 2,100, ambapo ekari 740 zilitengwa kwa ajili ya hifadhi.



Ameinisha wananchi 880 kutoka Vitongoji vya Mpera na Sokoine wanahusika katika zoezi la ulipaji fidia, na kuwataka wananchi kuepuka uvamizi wa eneo hilo.

Akizungumza kwa niaba ya wapokea fidia, Bi. Maina Elieza ameishukuru Serikali kwa wepesi wa mchakato wa ulipaji fidia ambao ulikwama tangu mwaka 1990.

Zoezi hilo ni sehemu ya hatua za Serikali za kulinda vyanzo vya maji nchini, kuhakikisha wananchi wanapatiwa haki ya stahiki na kuweka mazingira bora ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma.

.



MRADI WA HATI FUNGANI TANGA KAZI IWE SAA 24

Tanga, Tanzania

Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Maji wa Hati Fungani Tanga ametakiwa kuhakikisha anafanya kazi kwa saa 24 ili mradi ukamilike.

Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) ametoa maelekezo hayo akikagua mradi wa Hati Fungani Tanga unaoendelea katika eneo la Moe.

"Hatuna muda wa kupoteza, mkandarasi shinda eneo la kazi, Fedha ipo, hadi Novemba 2026 mradi uwe umekamilika na wananchi waanze kupata maji ya mradi huu," Aweso amesema

Amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo yake kwamba Taasisi za serikali ziwe na vyanzo mbadala vya fedha katika kutoa suluhu ya changamoto za watu, na kusema huu ni mradi wa mfano wa chanzo mbadala cha fedha na usimamizi wake usiwe wa kawaida na viongozi wanaudembelea mara kwa mara na kuahidi kuwa atarudi tena Oktoba 2026 ili kuhakikisha kazi inakamilika.





Mradi wa uboreshaji miundombinu ya maji wa Hati Fungani ya Kijani ya Tanga UWASA unathamani ya Shilingi bilioni 53.12 ambapo mpaka sasa utekelezaji wa mradi umefika zaidi ya asilimia 72 na utaanza kutoa huduma kwa wakazi wa Tanga Jiji, Muheza, Mkinga na Pangani mapema Novemba 2026.

Mradi wa Maji huo unajumuisha upanuzi wa mtandao wa mifumo ya majitaka katika Jiji la Tanga, ubadilishaji

wa kilomita 110 za mabomba chakavu ya maji, ufungaji wa Dira elfu 10 za malipo kwanza, upanuzi wa mtambo wa usambazaji maji kutoka Lita Milioni 45 Hadi kufikia Lita Milioni 60 kwa siku sambamba na ujenzi wa Tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji Lita milioni 35 ambapo itafanya maeneo yote ya Tanga Jiji, Muheza, Mkinga na Pangani kupata maji saa 24.



AWESO ATAKA MAJI GEITA KWA 100% OKTOBA 2026

Geita, Tanzania

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amesema hatokuwa kikwazo kwa wananchi kupata huduma ya maji safi na salama nchini.

Akikagua Mradi wa maji wa miji 28 katika eneo la tekeo la maji (Intake) mtaa wa Senga Geita amesema

atahakikisha kazi inafanyika kwa saa 24 ili kufikisha huduma ya maji kwa wananchi.



Mradi huo unatekelezwa kwa gharama Dola za Marekani Milioni 53.4 sawa na Shilingi za Tanzania Biilioni 124.

"Ninatambua Miundombinu ya sasa inauwezo wa kuzalisha Maji katika Manispaa ya Geita kwa wastani wa lita Milioni 9 kwa siku wakati mahitaji ni lita Milioni 22. Hivyo kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uzalishaji lita Milioni 45 kwa siku sawa na asilimia 100 ya mahitaji" Aweso amesema.

Kazi zilizo kamilika hadi muda huu ni ufungaji wa mitambo ikiwemo ufungaji wa Pampu 11 pamoja na Transforma nne.

Kwa sasa mradi utekelezaji wake umefika asilimia 82 ambapo hadi kufika Desemba 2026 maji yataanza kusukumwa katika matenki yote Matano yaliyojengwa (Mjini 2 na Vijijini 3) na wananchi kuanza kunufaika na huduma ya maji. Mradi u2tahudumia wananchi zaidi ya 716,948 kwa mji wa Geita.





HATIMAYE KILWA WAPATA MAJI YA MIJI 28

Kilwa, Tanzania

Mradi wa maji wa miji 28 Kilwa umeanza kunufaisha wananchi kupitia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali.

Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) amekagua mradi huo na kuona utekelezaji wake akielekeza maunganisho mapya ya huduma ya maji kwa wananchi wa Mavuji iwe siku Saba tu.

Mhe. Aweso akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mavuji, Kilwa Masoko, mkoani Lindi baada ya kufungua maji ya bomba ya mradi, amesisitiza kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira Kilwa Masoko (KIMUWASA) na Mamlaka za maji nchini huduma ya maunganisho ya maji majumbani isizidi siku Saba.

"Sasa niwasihi sana watendaji wa Wizara ya Maji mradi umekamilika na umeanza kutoa huduma, sasa maunganisho mapya yasizidi siku saba, sio mwananchi anaomba kuunganishiwa maji unamwambia njoo kesho, njoo kesho ili mradi atoe

kidogo dogo, hizo zilipendwa" Waziri Aweso amesema.

Mradi wa maji wa miji 28 Kilwa unathamani ya kiasi cha Shilingi za Tanzania Bilioni 44 na utekelezaji umefika asilimia 94.3 ambapo umeanza kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa kijiji cha Mavuji. Mradi huo utanufaisha wakazi zaidi ya 59,983 ambapo lita milioni 5.5 za maji zitazalishwa kwa siku kutoka mto Mavuji.



**SERIKALI KUPITIA WIZARA YA
MAJI NDANI YA KIPINDI KIFUPI
ITATOA KIASI CHA SHILINGI
MILIONI 508,300,000 ILI
KUKAMILISHA MRADI WA MAJI
WA ENDAMAGAY NA
GIDABOSHA ULIOPO BABATI.**

Manyara, Tanzania



Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), ametembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa huo wa thamani ya Shilingi bilioni 1.099 utakaonufaisha idadi ya watu 3,766 na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

Wakati wa ukaguzi wa mradi huo, Mhe. Aweso alisema Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maji ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa wakati.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 30, 2026, na utekelezaji umefika asilimia 87.

Waziri Aweso katika ukaguzi aliambatana na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge, Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), ambapo pia

amekagua miradi mbalimbali inayonufaishi jamii Mkoani Manyara.





GIZA HALIJAWAZUIA SOMANGA KUMPOKEA WAZIRI AWESO , ATOA MPANGO WA DHARULA

Somanga, Pwani

Serikali itaanza kuchimba idadi ya visima saba eneo la Somanga mkoani Lindi.

Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) amemuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri kutoa shilingi milioni 500 ili kazi ianze jumatatu, Septemba 28, 2026. Ametoa agiza hilo akiwa katika ukaguzi wa miradi ya maji mwishoni mwa mwezi Septemba 2026, mkoani Lindi.

Waziri Aweso amesema hayo akizungumza na wakazi wa Somanga walipomlaki barabarni nyakati za usiku wakati akiendelea na ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maji.

Mbunge wa Kilwa Kusini Mhe. Kinje kinjikitile alifikisha maombi ya kuchimbwa visima sita katika eneo hilo.

" Mhe.Mbunge Kinje umeomba vichimbwe visima sita, sasa mimi nakuongezea vitachimbwa saba. Nikuagize Katibu Mkuu hadi jumatatu hakikisha umeleta milioni 500 hapa Somanga na visima saba

vianze kuchimbwa ili kuongezea nguvu visima vilivyopo na wananchi wa Somanga wapate huduma ya maji bila usumbufu wowote" Waziri Aweso amesema.



KIASI CHA SHILINGI BILIONI 83.9 KINADAIWA KWA WATEJA MBALIMBALI WA HUDUMA YA MAJI NCHINI.

Bungeni, Dodoma



Kiasi hicho kimewasilishwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira katika kikao chake, Bungeni jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Jackson Kiswaga (Mb) akiongoza kamati hiyo pamoja na taratibu zitakazochukuliwa, kamati imeshauri na kuelekeza madai kufanyiwa kazi ili Serikali iendeele kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema moja ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuanza kutumika kwa matumizi ya Dira janja za malipo kabla ambapo deni hukusanywa kila malipo ya huduma ya maji yanapofanyika na kufanya mazungumzo na wadaiwa ili kuona namna bora ya kupunguza madai hayo.

Waziri Aweso amesainisha kuwa ili huduma ya maji imfikie mteja, nyuma yake zipo gharama kadhaa za uendeshaji ikiwemo nishati ya umeme, dawa za kutibu maji, rasilimaliwatu, na matengenezo.

Amesema mteja anapowajibika kulipa bili ni moja ya mchango wake katika kuimarisha na kuendeleza huduma ya maji nchini.





SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA HUDUMA YA MAJI

Bungeni, Dodoma

Uwekezaji unaofanywa na Serikali katika miradi ya maji ili kuhudumia wananchi umetoa matokeo kwa kuimarisha huduma ya maji katika jiji la Dodoma ambapo upatikanaji maji umeimarika kutoka asilimia 64.7 hadi asilimia 81.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema hayo akiwasilisha taarifa ya Upatikanaji maji na Usambazaji maji katika jiji la Dodoma kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, katika kikao Bungeni Dodoma.

Amesema jumla ya pampu za kusukuma maji 101 zinafanya kazi ya kufikisha huduma kwa wakazi wa Dodoma

Mhe. Aweso amesainisha Wizara ya Maji imepokea maelekezo yote ya Kamati na kujipanga kuwa bora zaidi katika huduma kwa jamii.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maji na Mazingira Mhe. Jackson Kiswaga (Mb), pamoja na mengine ameelekeza kazi zaidi ifanyike kupunguza upotevu wa maji (NRW) ambao umetoka asilimia 40 hadi asilimia 33 ili wateja zaidi wapate huduma ya maji kwa kuongeza mtandao wa huduma ya maji.



Mhe. Kiswaga amepongeza kazi kubwa inayofanywa na Serikali kufikisha huduma ya maji katika jamii na kusiondiza pamoja na miradi ya majisafi inayoendelea, teknolojia itumike katika usafi wa mazingira ili maji machafu yanayotibiwa yaweze kutumika katika shughuli za jamii ikiwamo kilimo na ujenzi.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) inahudumia wananchi, ikiwemo Bahi, Kongwa, Chamwino na Dodoma mjini.



MRADI WA MAJI WA MIJI 28, SERIKALI YAFIKISHA MAJI MANGAKA KWA ASILIMIA 100

Mangaka, Tanzania

Hatimaye mji wa Mangaka unaenda kunufaika na mradi wa maji wa mji 28 uliofanikishwa na Serikali ambapo hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi itakuwa asilimia 100.

Mradi hu oni mahsusi katika kuongeza uzalishaji na kusambaza maji katika mji wa Mangaka na maeneo ya vijijini vya wilaya ya Nanyumbu yanayopitiwa na bomba kuu hivyo kuondoa kabisa changamoto ya upatikanaji wa maji.

Mradi una uwezo wa kuzalisha maji lita milioni tano (5,000,000) kwa siku na kuhudumia wakazi wapatao 81,000 walioko Nanyumbu mjini na vijiji vinavyopitiwa na bomba kuu. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji inakuwa asilimia 100 katika mji wa Mangaka.

Thamani ya mradi wa miji 28 Mangaka ni takriban Dola za Marekani USD 16,380,000.59 na Serikali tayari imelipa Dola za Marekani USD 13,497,058.48.





Hivi sasa utekelezaji wa mradi umefika asilimia 96 na kwa kazi zifuatazo;

Ujenzi wa dakio (intake) umefika asilimia 96, Ujenzi wa mtambo wa kuchuja maji (WTP) upo asilimia asilimia 94, ulazaji wa bomba kubwa kutoka katika mtambo wa kuchuja maji (WTP) mpaka katika tanki la Sengenya umekamilika kwa asilimia 100, ulazaji wa mtandao wa kusambaza kwa maji kwa wateja upo asilimia 96 na ujenzi wa tenki (100m3) la kusambaza maji kijiji cha masuguru 94%

Majaribio ya kwanza na ya pili yameshafanyika ya kutoa maji kutoka kwenye dakio hadi tanki la kusambaza maji la Sengenya lenye ujazo wa lita milioni moja.. Hatua inayoendelea ni majaribio ya teknolojia ya scada pamoja na majaribio ya kusukuma maji yaliyotibiwa kutoka eneo la chujio (treatment plant) hadi kwenye mabomba ya usambazaji mjini Mangaka. Pia, majaribio mbalimbali ikiwemo majaribio ya line kubwa ya kutoa maji Masuguru kuelekea tanki la Sengenya.





Mradi wa Miji 28 unatekelezwa na Wizara ya Maji kupitia mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea (MANAWASA). Ni mradi mkubwa wa kutoa maji katika mto Ruvuma kuhudumia wakazi wa mji wa Mangaka pamoja na vijiji vyote vya pembezoni mwa mji na vijiji vinavyopitiwa na bomba kuu. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi kampuni ya M/S AFCON Infrastructure na mkandarasi mshauri WAPCOS LTD kutoka nchini India.

2026/2027

HOTUBA YA BAJETI 2026/2027



Jumanne ya tarehe 05 Mei, 2026, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb), aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2026/2027. Ufuatao ni muhtasari wa Bajeti hiyo ambayo imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26; Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP); Changamoto na hatua zinazochukuliwa; Vipaumbele na mwelekeo wa sekta kwa mwaka 2026/27, Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/27; na maombi ya fedha kwa mwaka 2026/27.



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Maji

HOTUBA YA BAJETI WIZARA YA MAJI 2026/2027

**Kusoma na Kupakua Hotuba ya Bajeti
Wizara ya Maji 2026/2027**

SCAN HAPA





Limeandaliwa na **Kitengo cha Mawasiliano**



Government City, Maji Street
P.o.box 456, Dodoma



Hotline :- +255 26 2322602



Fax No : +255 26 2322603



Email : Ps@maji.go.tz



Website ; www.maji.go.tz